UBAINIFU YAKINIFU

(kuhusu makosa ya kimanhaji na kielimu, yaliofanywa na baadhi ya wanaojinasibisha na maswala ya elimu)

MAKALA NO (4)

IMEANDIKWA NA:

ABUU IBRAAHIIM IBNU AL IMAAM

١٧/٤/١٤٣٨هـ

بسم الله الرحمن الرحيم.

الحمد لله رب العالمين، والصلاة والسلام على النبي الكريم، وعلى آله وأصحابه أجمعين.

أما بعد.

Baada ya kumshukuru Allah Mtukufu, na kumswalia Mtume wetu kipenzi, na Ahli zake, na Maswahaba wake wote:

Ndugu msomaji:

Katika makala namba moja, na mbili na tatu, tumefafanua usahihi kuwa neno Hizbu Llaah au Waliyyu Llaah hutumika kwa maana mbili, maana ya ujumla Inayoingia waislamu wote, na maana maalumu ya watu wema Ahlussunna wal jama'a wanaoshikamana na kumcha Allah.

Makala iliyopita tulielezea maana ya kwanza ya neno Waliyyu Llaah(mawalii wa Allah) ambapo tuliona Imaam Ibnul qayyim na Ibnu taimiyya wakibainisha maana hiyo na kuwa: kila muumini anaingia kwenye maana hiyo ya ujumla dhidi ya makafiri.

Na tukaona baadhi ya dalili zinazoonyesha hilo katika Qur'aan tukufu na tafsiri za wanachuoni wa

tafsiri katika hilo.

KWENYE MAKALA YA LEO: tutaona maana ya pili ya neno Waliyyu Llaa (mawalii wa Allah), nayo ni maana maalumu, ambayo hutumiwa tu kwa watu wa sunna na kushikamana na matendo mazuri na kuacha maovu dhidi ya watu wa bida'a na ufasiki na kadhalika.

Kwa maana haiwezekani kundi katika kundi la bida'a, au kundi katika kundi la watu wa maovu na ufasiki likaitwa mawalii wa Allah kwa maana hii maalumu, bali wao kwa zile bida'a zao wanaitwa watu wa bida'a na upotevu, na kwa ule uovu wao na maasi yao wanaitwa mafasiki na waovu.

Na maana hiyo maalumu, ndio aliitaja **Imaam Ibnul qayyim**-baada ya kutaja maana ya ujumla tuliyoitaja kwenye makala iliyopita- kwa kusema:

والولاية الخاصة: إن علم من نفسه أنه قائم لله بجميع حقوقه، مؤثر له على كل ما سواه في جميع حالاته قد صارت مراضي الله ومحابة هي همه ومتعلق خواطره يصبح ويمسي وهمه مرضاة ربه وإن سخط الخلق فهذا إذا قال أنا ولي الله كان صادقا

بدائع الفوائد لابن القيم ٣/٦٢١

"Na walaya (kupenda, nusra) ya Allah maalumu(mwenye sifa ya walaya hiyo) ni Yule ambaye akijijua nafsi yake kua ni mwenye kusimama kwa ajili ya Allah kwenye haki zake zote, ni mwenye kumtanguliza yeye dhidi ya kila kitu katika hali zote.

Ikawa kwake kupata radhi za Allah na mapenzi yake ndio hamu yake kubwa na ndio jambo lililogandana na mawazo yake.

Ana amka asubuhi na kushinda hadi jioni akiwa hima yake ni kupata radhi za mola wake hata kama viumbe watachukia, basi huyu (mtu mwenye sifa hizi) atakaposema: mimi ni walii wa Allah (kwa maana hii maalumu) atakua ni mkweli"

Tazama kitabu cha ibnul qayyim: badaai'ul fawaaid 3/621.

Tunaona hapa Ibnul Qayyim rahimahu Llaahu anafafanua aina ya walaya ya Allah ilio maalumu, nayo ni ile ambayo watu wake ni wenye imani ya juu na iliyotimia kutimia kunakotofautiana kati yao.

Kwani imani za mitume si sawa na imani za maswahaba, imani za maswahaba si sawa na imani za waliokuja baada yao.

Pia imani za mitumi wenyewe kwa wenyewe hutofautiana, pia imani za maswahaba wenyewe kwa wenyewe hutofautiana, na mfano wake, na wote hao wanaingia katika watu wenye imani za juu zilizotimia.

Na maana hii pia ameiashiria Sheikhul Islaam Ibnu taimiyya rahimahu Llaahu, alipokua akibainisha daraja tatu za waislamu waliotajwa katika suuratul faatwir aya ya 32.

Ambapo kundi aliloanza kulitaja Allah ni la waislamu wanaofanya mema na mabaya (hawa wemeitwa wenye kizudhulumu nafsi zao).

Na hawa ndio wale ambao wanaingia kwenye walaya ya Allah ya ujumla na hawaingii katika walaya ya Allah maalumu.

Kundi la pili: ni waislamu ambao wanatekeleza ibada zote za faradhi na kuacha mabaya (hawa wameitwa muqtaswiduuna).

Kundi la tatu: ni waislamu ambao wanatekeleza ibda zote za faradhi na sunna, na kuacha yote ya haramu na yenye kuchukiza na wakifanya maasi haraka sana hututubu kwa mola wao.

(hawa wameitwa assaabiquuna bil khairaat, yani waliotangulia kwenye kheri).

Na hili kundi la pili na la tatu: ndio mawalii wa Allah kamilifu, lakini wenyewe wametofautiana kwenye huo ukamilifu, assaabiquuna ni wakamilifu zaidi ya muqtaswiduuna.

Na hii ndio maana ya maneno ya Ibnu taimiyya aliposema- baada ya kutaja kundi la pili na la tatu-:

وَكُلٌّ مِنْ الصِّنْفَيْنِ الْمُقْتَصِدِينَ وَالسَّابِقِينَ مِنْ أَوْلِيَاءِ اللَّهِ الَّذِينَ ذَكَرَهُمْ فِي كِتَابِهِ بِقَوْلِهِ : {أَلَا إنَّ أَوْلِيَاءَ اللَّهِ لَا خَوْفٌ عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ يَحْزَنُونَ } { الَّذِينَ آمَنُوا وَكَانُوا يَتَّقُونَ } فَحَدُّ أَوْلِيَاءِ اللَّهِ : هُمْ الْمُؤْمِنُونَ الْمُتَّقُونَ.

مجموع الفتاوى لابن تيمية ٦/١٠

"Na makundi yote mawili (muqtaswiduuna na Assaabiquuna bil khairaat) ni katika mawalii wa Allah

(waliokamilika) ambao amewataja Allah katika kitabu chake kwa kusema:

Jueni, hakika mawalii wa Allah hawana khofu juu yao na hawana huzuni (mawalii hao waliokamilika) ni wale ambao wameamini na wakawa wachamungu (kikamilifu). Basi mipaka ya mawalii wa Allah: ni wale ambao wameamini na ni wachamungu"

Tazama maj'mu'ul fata'wa ya Ibnu Taimiyya 10/6.

Kisha akabainisha Ibnu taimiyya kuwa mawalii hao wenye maana maalumu wako makundi mawili yaliotofautiana ukamilifu wao.

Ambayo moja ameliita la ujumla linaloingia kila ambaye anafanya faradhi zote na kuacha ya haramu yote, ambalo ndilo lililoitwa: **muqtaswiduuna**.

Na la pili ni maalumu. nalo ni lile la wale ambao wamefanya ya faradhi yote na ya sunna, na kuacha ya haramu yote na yenye kuchukiza (makruuh) na hili ndilo kundi la juu kabisa, la Mitume na maswiddiiqiina.

Ufafanuzi huo wa Ibnu Taimiyya ni huu **ambapo alisema:**

وَلَكِنَّ ذَلِكَ يَنْقَسِمُ : إلَى " عَامٍّ " وَهُمْ الْمُقْتَصِدُونَ ، وَ " خَاصٍّ " وَهُمْ السَّابِقُونَ وَإِنْ كَانَ السَّابِقُونَ هُمْ أَعْلَى دَرَجَاتٍ كَالْأَنْبِيَاءِ وَالصِّدِّيقِينَ

مجموع الفتاوى لابن تيمية ١٠/٦-٧.

" lakini hao (mawalii wenye maana maalumu iliotimia) wamegawanyika makundi mawili, kundi la kwanza ni la ujumla, nalo ni wale muqtaswiduuna (waliotekeleza faradhi zote na kuacha haramu zote).

Na kundi la pili, ni kundi maalumu, nalo ni lile la Assaabiquuna bil khairaat (nao ni wale waliotekeleza faradhi zote na sunna zote na kuacha haramu zote na makruuhaati yote).

pamoja nakua hao Assaabiquuna ndio kundi lenye daraja ya juu kabisa, kama vile mitume na maswiddiiquuna"

Tazama maj'mu'ul fatawa ya Ibnu Taimiyya 10/6-7.

Tunaona hapo, kuwa Imaam Ibnu Taimiyya aliongelea watu wanaoitwa mawalii wa Allah kwa maana maalumu.

na kuwa watu hao wenyewe wametofautiana daraja zao za uwalii, wako wa juu kabisa, na wako wa chini kidogo.

lakini wote ni wenye imani kamilifu kwa kufanya yote ya amri na kuacha makatazo yote.

Ama wale waislamu wanaofanya mema na maovu ambao wameitwa (wenye kuzidhulumu nafsi zao): hao hawaingii kwenye kuitwa mawalii wa Allah kwa maana maalumu iliyokamilika.

Lakini pia hawatoki kwenye walaya ya Allah moja kwa moja, bali wanakua na sehemu ya walaya ya Allah kulingana na imani yao na taq'wa yao, na wanakua na uadui wa Allah kulingana na bida'a zao na maasi yao.

na hawa huingia kwenye walaya ya Allah ya ujumla inayotafautisha waislamu dhidi ya wasiokua waislamu.

Na ndio maana baada ya kubainisha hiyo walaya maalumu: Ibnu Taimiyya chini yake kwenye huo ukurasa, akawabainisha hawa waislamu wenye

mema na maovu kwa kusema:

أَمَّا الظَّالِمُ لِنَفْسِهِ مِنْ أَهْلِ الْإِيمَانِ : فَمَعَهُ مِنْ وِلَايَةِ اللَّهِ بِقَدْرِ إِيمَانِهِ وَتَقْوَاهُ كَمَا مَعَهُ مِنْ ضِدِّ ذَلِكَ بِقَدْرِ فُجُورِهِ

مجموع الفتاوى لابن تيمية ٧/١٠

"Ama mwenye kuidhulumu nafsi yake katika watu wa imani (waislamu): mtu huyo ana sehemu katika walaya (nusra na mapenzi) ya Allah kwa kadri ya imani yake na uchamungu wake, kama ambavyo ana kinyume chake (yani uadui wa Allah) kwa kadri ya uovu wake".

Ama dalili za maana hii maalumu iliyokamilika ya neno(waliyyu Llaah) ni nyingi sana, lakini nitataja mbili tu inshaa Allah.

KWANZA: ni qauli yake Allah mtukufu aliposema katika suurat yuunus, aya ya 62 mpaka 64:

أَلا إِنَّ أَوْلِيَاءَ اللَّهِ لا خَوْفٌ عَلَيْهِمْ وَلا هُمْ يَحْزَنُونَ (٦٢) الَّذِينَ آمَنُوا وَكَانُوا يَتَّقُونَ (٦٣) لَهُمُ الْبُشْرَى فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَفِي الآخِرَةِ لا تَبْدِيلَ لِكَلِمَاتِ اللَّهِ ذَلِكَ هُوَ الْفَوْزُ الْعَظِيمُ

"Jueni, hakika mawalii wa Allah ni wale ambao hawana khofu juu yao, na wala hawahuzuniki. Ni wale ambao wameamini na wakawa wachamungu.

Wana bishara njema katika maisha ya duniani na akhera pia,hakuna kubadilika katika maneno ya Alla,

hakika huko ndiko kufuzu kuliko kukubwa"

Hakuna shaka kua Aya hizi zinazungumzia mawalii wa allah wenye maana maalumu, nao ni wale watendao mema na kuacha mabaya yote.

kwani hawezi kuambiwa hana khofu wala huzuni muislamu ambaye ni mtu wa bida'a, au muislamu ambaye ni fasiki, kwani watu wa bida'a na mafasiki wameonywa na adhabu ya Allah, kwa kadri ya bida'a zao na ufasiki wao.

NA DALILI NYINGINE: inayozungumzia mawalii wa Allah kwa maana maalumu, ni hadiith qudusiy ambapo Allah mtukufu: anatahadharisha wanaowafanyia uadui mawalii wake, ambao ni wenye kujikurubisha kwake kwa kutekeleza maamrisho ya faradhi na sunna.

Hadithi hiyo ni maarufu ameopokea Imaamul bukhaary katika sahihi yake.

Kwahiyo dhahiri ya Aya na hadithi hiyo zinazungumzia mawalii wa Allah kwa maana

maalumu, ya waislamu walioshikamana na sunna na kumcha Allah, kwa kutekeleza faradhi na kuacha haramu zote.

Ama watu wa bida'a na mafasiki ambao hawajakufuru kwa bida'a zao na ufasiki wao, hao wanaingia katika maana ya ujumla ya Auliyaau Llaah (mawalii wa Allah) wanapotajwa waislamu dhidi ya wasiokua waislamu.

Na ndio maana Al Imaamu Attwahaawiy katika Aqida yake akasema:

والمؤمنون كلهم أولياء الرحمن، وأكرمهم عند الله أطوعهم وأتبعهم للقرآن

"Na waumini wote ni mawalii wa Allah, na watakao kirimiwa zaidi mbele ya Allah ni wale wachamungu zaidi na wanaofuata Qur,aan zaidi"

Amesema Al Allaamah **Swaaleh Alfauzaan** Allah amhifadhi- akisherehesha maneno hayo ya Al Imaam Attwahaawy-:

هذا حق، فالمؤمنون كلهم أولياء الله، يعني: أحبابه، فالله يحب المؤمنين، ويحب المتقين، ويحب المحسنين، ويحب التوابين، ويحب المتطهرين، كما أنه يبغض الكافرين، ويبغض الفاسقين، فالله يحب ويبغض على الأعمال. فكل مؤمن يكون وليا لله، وتتفاضل الولاية بعضهم أفضل من بعض.

"Hii ni haki, waumini wote ni mawalii wa Alla, yani ni wapendwa wake, kwani Alla anawapenda waumini, na anawapenda wachamungu, na anawapenda muhsinuuna, na anawapenda wenye kutubia, na anawapenda wenye kujitwaharisha.

kama vile ambavyo Alla anawachukia makafiri, anawachukia mafasiki, kwahiyo Allah anampenda (muislam) na anamchukia kulingana na matendo yake.

Kwahiyo kila muumini anakua ni walii wa Allah, na walaya zinatofautiana, baadhi yake ni bora kuliko zingine"

Kisha Al Allaama Al fauzaan akaleta zile aya tulizoleta hapo juu za suurat yuunus aya ya 62-63

kisha akasema:

فمن الناس من ولايته مع الله تامة، ومنهم من ولايته مع الله ناقصة، ومنهم من هو عدو الله بعيد عن الله سبحانه وتعالى، فكل من فيه إيمان وتقوى فهو ولي الله، ولكن الولاية تتفاضل بحسب الأعمال، فمنهم من ولايته كاملة، ومنهم من هو ولي من وجه، وهو المؤمن الفاسق، ولي لله بطاعته، عدو الله بمعصيته ومخالفته. ومنهم من هو عدو خالص كالكافر والمشرك، هذا هو الحق.

انظر: التعليقات المختصرة على متن العقيدة الطحاوية للشيخ صالح الفوزان ص ١٥١-١٥٢ دار العاصمة.

"Kwa hiyo, miongoni mwa watu, wako ambao

walaya(nusra na mapenzi) ya Allah kwao yametimia, na wako ambao walaya yao kutoka kwa Allah ni pungufu, na wako ambao ni maadui wa Alla, wako mbali na Allah mtukufu.

Kwahiyo, kila ambaye ana imani na uchamungu, basi yeye ni walii wa Allah, lakini walaya inatofautiana kwa ubora kulingana na matendo.

wako ambao walaya yao kutoka kwa Allah ni kamili, na wako ambao ni mawalii kwa upande flani(na kwa upande mwingine ni maadui wa Allah).

Nao ni waumini (waislamu) ambao ni mafaasiki, (wao) ni mawalii wa Allah kwa twa'a (uchamungu) wao, na ni maadui wa Alla kwa maasi yao, na kukhalifu kwao.

na wako ambao ni maadui moja kwa moja (hawana sehemu ya walaya hata kidogo), nao ni makafiri na washirikina, hii ndio haki"

Tazama yote hayo kwenye kitabu cha Shekh Fauzani cha sherehe yake kwa mukhtasari ya kitabu cha Imaam Attwahaawiy, uk: 151- 152.

Maneno hayo ya Imaamu ttwahaawiy yako wazi ndugu msomaji, kua: waumini wote ni mawalii wa Allah, na akabainisha kuwa, mbora katika wao ni Yule mchamungu zaidi.

akimaanisha wale wenye uwalii kamili, kwa kufanya matendo mazuri na kuacha mabaya yote, hawa ni mawalii kamili, na ndio wanaoitwa mawalii kwa maana maalumu.

Ama wanaofanya mema na maovu, hawa japo hawaitwi mawalii kwa maana maalumu, ila wanaingia katika mawalii wa Allah katika yale mema, na hawaingiia kwenye mawalii wa Alla katika maovu yao.

Na kafafanua Al Allaamah Alfauzaan,bali ameweka wazi zaidi kwa kusema kuwa: adui wa moja kwa moja asiyekuwa na walaya ya Alla ya nusra na kuwapenda: ni kafiri na mshirikina.

Je, kwa ufafanuzi huu, wa wanachuoni wa kisalafy, ulio sheheni dalili mbali mbali, bado Abdurrah'maan ataendelea na maneno yake? Ya kudai kua:

Si kila muislamu anaingia katika mawalii wa Allah? Bado hajagundua tu kua aliingia kwenye makosa ya kiitikadi?

Na je, sasa atakubali kua neno Hizbu Llaah linaingia kwa waislamu wote kwa maana ya ujumla, na pia linatumika kwa baadhi ya waislamu(Ahlussunna na wamchao Allah) kwa maana maalumu?

Ndugu msomaji: japo nina uhakika kua maudhui hii imeeleweka sana Inshaa Allah: ila kuna ufafanuzi muhimu-unaohusiana na maudhui hii hii-tutaufafanua katika makala **NAMABA TANO** Inshaa Allah.

Ikiwemo kuona maneno muhimu ya mwanachuoni mkubwa Asshekh Swaaleh Aalu ssheikh Allah amhifadhi katika ufafanuzi wa maneo ya Al Imaam Attwahaawi kuwa(waumini wote ni mawalii wa Alla)

Pia kufafanua maneno ya Assheikh Ibnu othaimiin kuwa walaya ya Allah imegawika sehemu mbili:

inayowahusu waislamu na wasio waislamu, na inayowahusu waislamu tu.

pamoja na kumalizia na maneno mengine ya Shekh Muqbil na shekh Ibnu Othaimiin kuhusu Hizbu LLaah na Hizbu sshaitwaan.

IMEANDIKWA NA:

ABUU IBRAAHIIM IBNU AL IMAAM
وفقه الله وغفر له ولوالديه ولجميع المسلمين.

١٤٣٨/٤/١٧